

# Litoe Somali

Kondo hulipiwa kondo, ni kauli toka zama,  
Ilianza kwa mawindo, ya insali si wanyama,  
Kuuwana kwa manyundo, mashoka na vis-  
erema,  
Amiri Bwana Uhuru, litoe kesho Somali.

Kenya tunaomboleza, hivi vifo vya kinyama,  
Kwa hisani lijitoza, kukomoa palokwama,  
Somali kuipenyeza, kukomboa nchi nzima,  
Amiri Bwana Uhuru, litoe jeshi Somali.

Mataifa yaungama, kuhawini kwa ujima,  
Somali irudi pema, pa kuishi wanadama,  
Wamerika walihema, hatimaye wakahama,  
Amiri Bwana Uhuru, litoe jeshi Somali.

Kenya ilijizatiti, Somali yeze simama,  
Yajitowa kwayo dhati, magaidi kuwazima,  
Matokeyo ni majuti, yawo wetu huno wema,  
Amiri Bwana Uhuru, litoe jeshi Somali.

Leo yino tunalia, katokea tena njama!  
Letu jeshi kangamia, idadi kubwa kakoma,  
Mchangani katulia, ya peponi yawe mema,  
Amiri Bwana Uhuru, litoe jeshi Somali.

*Ramadhan Abdallah Savonge,  
"Malenga wa Nchi\_Kavu"  
Chuo Kikuu SEKU, Kitui*